



Mratibu Mtendaji wa Shirika la UNV atembelea Tanzania

Umoja Toleo Na. 83
Machi - Aprili 2019



Mratibu Mtendaji wa UNV, Bw. Olivier Adam (kushoto), akipokea zawadi kutoka wa Rais wa Zanzibar, Mh. Dkt. Ali Mohamed Shein (kulia) alipomtembelea katika Ikulu ya Zanzibar. **Picha | Ikulu**

Vidokezo

- Wanaume wanaofanya kazi kwa bidii kuhakikisha uzazi salama katika kambi za wakimbizi nchini Tanzania
- UN, Serikali Zahusisha Vyama vya Kiraia kuhusu SDGs
- Siku ya Kimataifa ya Wanawake: Serikali yatoa wito wa kupanua uwezeshaji wanawake kiuchumi

mipango ya maendeleo na kiutu—ikiwemo kuwahifadhi zaidi ya wakimbizi 300,000 kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Burundi.

Kwa kuwa na wanaojitolea 77 walio katika Mashirika yote ya UN, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kujitolea (UNV) linashirikiana na jamii ili kutafuta suluhu za kudumu katika sekta mtambuka kadhaa zikiwemo afya, elimu, uwezeshaji wanawake kiuchumi, na kumaliza ukatili wa kijinsia.

Inaendelea ukurasa wa 2

Huku ikiwa na zaidi ya watu milioni 50 na ikipakana na nchi nane tofauti—haitakuwa makosa kwamba Jamhuri ya Tanzania ni nchi yenye umuhimu mkubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki. Umoja wa Mataifa una mchango mkubwa nchini Tanzania ambako mashirika 23 ya UN yanashirikiana kwa karibu na serikali katika kutekeleza

Kauli ya Serikali

“Pia ningependa kutumia fursa hii kutoa shukurani kwa ... mashirika ya UN, yakiwemo UN Women, UNFPA, UNICEF na UNDP kwa juhudi zao endelevu za kusaidia ufikiwaji wa Usawa wa Jinsia kwa ajili ya Maendeleo Endelevu.”

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mh. Ummu Mwalimu, alipokuwa akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake huko Mwanza mnamo Machi 8, 2019.

Inatoka ukurasa wa 1

Wakati wa ziara yake nchini Tanzania, ili kuzindua rasmi ziara yake ya Afrika Mashariki, Mratibu Mtendaji wa UNV, Bw. Olivier Adam, alipata nafasi ya kukutana na wanaojitolea hawa na kusikiliza simulizi zao jinsi wanavyotekeleza majukumu yao na changamoto wanazokabiliana nazo.

Pia alikutana na Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa na wakuu na wawakilishi wa Mashirika ya UN ambapo aliihimiza Timu ya Nchi ya UN kufungua milango zaidi kwa utaratibu wa kujitolea kwani asilimia 80 ya wanaojitolea 77 waliopo wako zaidi katika

mashirika mawili—UNDP na UNHCR. Bw. Adam alirejea ahadi ya UNV ya kushirikiana na mashirika ya UN ili kusukuma mbele vipawa na utayari wa wanaojitolea katika kuimarisha matokeo ya programu zilizopo za nchi.

Wakati wa ziara yake nchini Tanzania, Mratibu Mtendaji huyu pia alitembeleza Zanzibar ambako alikutana na Rais wa Zanzibar, Mh. Dkt. Ali Mohammed Shein, na kupata fursa ya kujadiliana naye kuhusu namna UNV inavyoweza kusaidia vipewaumbele vya maendeleo vya Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar. Miongoni mwa maeneo yenye uwezekano wa ushirikiano ambayo Rais aliyaangazia ni pamoja na kutafuta watu wanaojitolea ili kusaidia katika kufundisha masomo ya sayansi na hisabati mashuleni ambako hivi sasa kuna upungufu na kutoa ujuzi wa kitaalamu mahospitalini ili kujenga uwezo wa kuleta utaalamu wa kina katika maeneo kama upasuaji wa mifupa. Viongozi hao wawili walijadiliana uwezekano wa kuingiza watu wanaojitolea katika kituo cha malezi ambako wanaojitolea wangeweza kuwasaidia wanawake na vijana kuendeleza stadi za ujasiriamali.

Mtukufu Binti Mfalme Sarah Zeid Atembelea Tanzania



Mshauri Maalumu wa Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Mtukufu Binti Mfalme Sarah Zeid (kushoto) akiwatembelea wanufaika wa mradi wa lishe wa 'Boresha Lishe' unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya huko mkoani Dodoma. **Picha | Zainul Mzige**

Mwishoni mwa mwezi Machi, Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) lilikuwa mwenyeji wa Mtukufu Binti Mfalme Sarah Zeid wa Jordan. Binti Mfalme Sarah ni mshauri maalumu wa masuala ya afya ya mama WFP na mtetezi wa lishe bora katika siku 1,000 za mwanzo za maisha ya mtoto.

Wakati wa ziara yake, alikutana na maofisa wa Serikali na wadau wa masuala ya lishe na kujadiliana nao kuhusu kuunda ushirika unaoweza kuchangia katika kumaliza utapiamlo nchini Tanzania.

Vilevile, Binti Mfalme alitembelea Mradi wa Boresha Lishe huko Dodoma ambako alikutana na

wanufaika wa mradi, alishuhudia vikundi vya ukopeshaji na kuona mlo maalumu ukigawiwa kwa wanawake wajawazito na wanaonyonyesha. Programu hiyo inatekelezwa na WFP kwa kushirikiana na Shirika la Save the Children kupitia ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU).



Washirika wa Maendeleo, maafisa wa Serikali na wanakamati ya maandalizi ya Baraza la Vijana la Umoja wa Mataifa ya Tanzania (TIMUN) wakati wa sherehe za kufunga tukio. *Picha | Grace Mongi /UN Tanzania*

Mwaka huu, zaidi ya vijana 200 kutoka nchini na mataifa mengine walishiriki katika jumuiko la kila mwaka linalojulikana kama Baraza la vijana la Umoja wa Mataifa (TIMUN) lililofanyika mkoani Morogoro mwishoni mwa mwezi Aprili.

Mkutano wa TIMUN wa mwaka huu uliweka mkazo katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na kuangazia kwa namna ya kipekee ushiriki wa vijana katika Lengo la 3 (Afya Bora & Hali Njema ya Maisha), Lengo la 13 (Mabadiliko ya Tabia ya Nchi) na Lengo la 16 (Amani, Haki na Taasisi Imara).

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo, mratibu wa shughuli na mjumbe wa Kluba ya Vijana wa Umoja

wa Mataifa (YUNA), Bw. Kelvin Edward alisema: “Nimefurahi kuona kuwa kuna washiriki wengi katika mkutano wa mwaka huu—na wote hawa wamedhamiria kuona kwamba vijana wa leo na kesho wanawezeshwa, wanajumuishwa na wanapewa nafasi sawa. Ninawashukuru UN Tanzania, yakiwemo mashirika ya UNICEF na UNFPA na pia wadau wengine wanaotuunga mkono, kwa kutupatia jukwaa hili ili vijana wapate fursa ya kushirikisha juhudi na ubunifu wao hasa tunaposhirikiana katika kutekeleza Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu. Wakati wote wa mkutano huu, vijana watapata fursa ya kueleza maoni yao, matumaini na mashaka yao kuhusu siku zijazo.”

Akizungumza kwa niaba ya UN
Inaendelea ukurasa wa 4

“Ni jambo lakupendeza kuona mkusanyiko wa mabalozi vijana wenye hamasa kubwa, hii ni ishara ya ushiriki wa vijana katika utekelezaji wa SDGs na pia kuimarisha maendeleo ya kiuchumi ya nchi.”

-Bw. Deusdedit Kaganda, Kaimu Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Pande Nyingi kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki



Kama sehemu ya mwaka huu ya Baraza la vijana la Umoja wa Mataifa ya Tanzania (TIMUN), wajumbe walifanya ziara ya kueneza SDGskatika Shule ya Sekondari ya Morogoro. **Picha | Grace Mongi /UN Tanzania**

Tanzania wakati wa uzinduzi
Inatoka ukurasa wa 3

wa mkutano, Afisa wa Habari kutokea kituo cha habari cha Umoja wa Mataifa, Bi. Nafisa Didi alisema kwamba UN itaendelea kusaidia ushirikishwaji wa vijana katika utekelezaji wa SDGs. Alisema: “Vijana wanaunda asilimia kubwa ya idadi ya watu. Ni muhimu kwamba wawe wanapata taarifa na kushirikishwa katika utekelezaji wa SDGs, hasa sasa ambapo tuko mwaka wa nne wa utekelezaji wa ajenda hiyo. Tungependa kila kijana pale alipo kushirikishwa katika kufuatilia na kutoa taarifa za maendeleo.”

Wakati wa matukio ya siku tano, kulikuwa na uwasilishaji kutoka mashirika mbalimbali, mengine yakiwa ya UN, yanayojishughulisha na vijana. Akizungumza wakati wa kufungwa kwa mkutano huo, Kaimu Mkurugenzi wa

Ushirikiano wa Pande Nyingi kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Bw. Deusdedit Kaganda alisema: “Ni jambo la kupendeza kuona mkusanyiko wa mabalozi vijana wenye hamasa kubwa, hii ni ishara ya ushiriki wa vijana katika utekelezaji wa SDGs na pia kuimarisha maendeleo ya kiuchumi ya nchi.” Tukio la kufunga mkutano huo lilishuhudiwa pia na mwakilishi kutoka Ubalizi wa Marekani, Bw. Jeff Ladenson na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Bw. Kebwe Steven Kebwe.

Mkutano wa TIMUN, ambao huandaliwa na Vijana wa Umoja wa Mataifa (YUNA), huandaliwa kila mwaka na kuwaleta vijana kutoka kote ulimwenguni. Mkutano wa mwaka huu ulifadhiliwa na UN Tanzania, Ofisi ya Waziri Mkuu, UNICEF, UNFPA, UNIC, Ubalizi wa Marekani, Pathfinder, Plan International na Taasisi ya Kimataifa ya Vijana.

“Vijana wanaunda asilimia kubwa ya idadi ya watu. Ni muhimu kwamba wawe wanapata taarifa na kushirikishwa katika utekelezaji wa SDGs, hasa sasa ambapo tuko mwaka wa nne wa utekelezaji wa ajenda hiyo. Tungependa kila kijana pale alipo kushirikishwa katika kufuatilia na kutoa taarifa za maendeleo.”

**- Bi. Didi Nafisa,
Afisa wa Habari
Umoja wa Mataifa**



Wanagenzi wakishiriki katika mijadala ya makundi na kushirikishana ujuzi wkati wa mafunzo ya ujuzi wa kidijitali yaliyoandaliwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa ajili ya wahitimu wa uanagenzi huko Arusha. **Picha | ILO**

Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT), Chama cha Wenye Hoteli Tanzania (HAT) na Chama cha Waajiri cha Tanzania (ATE) liliandaa warsha ya mafunzo ya ujuzi wa kidijitali huko Arusha mwishoni mwa mwezi Machi. Warsha hiyo ni sehemu ya mpango wa ILO wa kuimarisha uendelezaji wa ujuzi na kuongeza uwezo wa kuajiriwa wa vijana wa Tanzania. Pia ni mpango unaolenga kuchangia katika hatua za kimkakati za kuchukua ili kuimarisha uwezo wa sasa wa watu na taasisi kwa kutoa zana na uzoefu kupitia ushiriki wa moja kwa moja.

Walilengwa katika mpango huo ni wahitimu wa programu ya uanagenzi (mafunzo kazini) ambao tayari wamemaliza masomo yao na sasa wako

katika kipindi cha mpito kuelekea kwenye ajira kamili au kujiajiri, lengo la mafunzo likiwa ni kuimarisha ujuzi wa mawasiliano ya mtu na mtu ya wahitimu hawa na ujuzi wa mawasiliano ili kuwaandaa vizuri zaidi na soko la ajira.

Mradi huo unafadhiliwa na Serikali ya Norway na unatekelezwa na ILO kwa kushirikiana kwa karibu na taasisi zilizotajwa hapo mwanzo na wadau kutoka sekta binafsi. Washirika wa sekta binafsi walioshiriki wamebainisha ujuzi wa kidijitali kama eneo ambalo kwalo wahitimu wa uanagenzi wanahitaji mafunzo zaidi. Kwa mfano, ujuzi wa mawasiliano na uongozi ulitajwa na waajiri kama maeneo yanayohitaji kuimarishwa zaidi.

Baadhi ya maeneo yaliyofundishwa wakati wa

mafunzo ni pamoja na huduma kwa mteja na utoaji wa huduma, usimamizi, huduma za ujasiriamali na uanzishwaji wa huduma za biashara (BDS) na kutoa elimu kuhusu fursa za kibiashara..

Akiwahutubia wanagenzi, Meneja Mkuu wa Hoteli ya Melia, (ambaye ni mshirika wa muda mrefu wa programu hii), Bw. Nicolas Konig, aliipongeza ILO kwa kutoa mafunzo hayo kwa vijana ambao ndio watu sahihi kwa ajili ya fursa za sasa za ajira katika hoteli kubwa nchini.

Mafunzo hayo ni sehemu ya programu ya awamu tatu kwa Arusha, Dar es Salaam na Zanzibar kama sehemu ya msaada wa ILO kwa juhudi za serikali za kuhamasisha mafunzo ili kutoa ujuzi na kupata fursa za ajira zinazowalenga zaidi ya vijana na wanawake 200.

Ujumbe Mkuu katika Siku ya Kimataifa ya Misitu



Kuwajengea watoto msingi bora wa kuelewa manufaa muhimu ya misitu ni hatua muhimu ya kulinda rasilimali za asili kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Picha | FAO Tanzania

Mwanzoni mwa mwezi Machi, Tanzania iliungana na ulimwengu ili kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Misitu ambapo ujumbe mkuu ulikuwa: 'Misitu na Elimu'. Siku hii, ambayo ilitangazwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa tangu mwaka 2012, inaadhimisha na kutoa elimu kuhusu aina zote za misitu.

Katika kila Siku ya Kimataifa ya Misitu, nchi huandaa sherehe za mahali, kitaifa na kimataifa zinazohusisha masuala ya misitu na miti, kama vile kupanda miti na kampeni za utoaji elimu. Hapa nchini Tanzania, wadau mbalimbali, ikiwemo Serikali kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) iliyo chini ya Wizara Maliasili na Utalii na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), miongoni mwa wengine, huandaa shughuli mbalimabli kuadhimisha siku hii.

Katika tamko lake, Mwakilishi wa FAO nchini Tanzania, Bw. Fred Kafeero, alisisitiza umuhimu wa misitu kwa mazingira ya dunia. "Umuhimu wa misitu

unafahamika vema kwani uhai wote hapa duniani, yaani hata wa kwetu, unategemea uwepo wa misitu. Hii ndiyo inayotoa njia za kujipatia riziki kwa binadamu; ni muhimu kwa ajili ya makazi ya wanyama, inalinda vyanzo vya maji; inazuia mmomonyoko wa udongo; na inasaidia kukabiliana na madhira ya mabadiliko ya tabia ya nchi," alisema.

Hata hivyo, alieleza kuwa licha ya ukweli huu, katika ngazi ya dunia, misitu imekuwa ikitoweka kwa kasi kubwa ambayo haijawahi kutokea kabla. Bw. Kafeero alirejelea ripoti ya Tathmini ya Rasilimali Misitu Duniani ya 2015 (Global Forest Resources Assessment 2015) inayoonyesha kwamba mwaka 1990, dunia ilikuwa na hekta milioni 4,128 za misitu, lakini kufika maka 2015, zilikuwa zimepungua hadi kufika hekta milioni 3,999.

Nchini Tanzania, ripoti ya Usimamizi na Thamini ya Rasilimali Misitu za Taifa ilikadiria kuwa kasi ya mwaka ya kupotea kwa misitu ilikuwa ni hekta 372,816, wakati ambapo

makadirio yaliyofanywa na Kituo cha Taifa cha Kusimamia Hewa ya Ukaa yaliyonyesha ongezeko la kiasi cha kasi ya kupotea kwa misitu kwa hekta 469,420.

"Kama ujumbe mkuu wa Siku ya Kimataifa ya Misitu ya 2019 unavyosema kuwa Misitu na Elimu, yatupasa kutafakari umuhimu wa elimu ya misitu katika kukabiliana na changamoto za sasa na baadae," aliasa Bw. Kafeero.

Elimu imetambuliwa muda mrefu kama njia kuu ya kujenga ushawishi kwenye maarifa, ujuzi na amali za raia ili kuunga mkono maendeleo endelevu. Kuwapa watoto msingi wa kuelewa vizuri umuhimu mkuu wa misitu ni jambo muhimu sana ili kulinda rasilimali hizi kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Misitu bora ni jambo muhimu sana katika azma yetu ya kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

"Umuhimu wa misitu unafahamika vema kwani uhai wote hapa duniani, yaani hata wa kwetu, unategemea uwepo wa misitu. Hii ndiyo inayotoa njia za kujipatia riziki kwa binadamu; ni muhimu kwa ajili ya makazi ya wanyama, inalinda vyanzo vya maji; inazuia mmomonyoko wa udongo; na inasaidia kukabiliana na madhira ya mabadiliko ya tabia ya nchi,"

**- Bw. Fred Kafeero,
Mwakilishi wa FAO nchini
Tanzania**

Wanaume wanaofanya kazi kwa bidii kuhakikisha uzazi salama katika kambi za wakimbizi nchini Tanzania



Mmoja wa wanawake waliojifungua mtoto wake katika Kituo cha Afya cha Nyarugusu ambacho kinasaidiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) mkoani Kigoma. *Picha | UNFPA*

Toka zama na zama, suala la afya ya uzazi na ya mama limechukuliwa kama suala la akina mama, lakini wanaume nao wana nafasi muhimu. Kutana na Abdul Nyamguma na Hofne Chrisostom Yohana, wawili hawa ni miongoni mwa manesi na wakunga 15 wanaotekeleza programu iliyofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) ili kutoa matunzo kamili ya mama na mtoto katika Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu iliyoko huko mkoani Kigoma, Tanzania. Takribani watoto 10,000 wanazaliwa katika kambi tatu za mkoani Kigoma, na mahitaji ya huduma za afya yako juu. Katika siku ya kawaida katika chumba cha uzazi, Hofne huwapokea wagonjwa wa kulazwa, huchukua taarifa zao za mahudhurio ya

kliniki kabla ya kuzaa, takwimu muhimu, na kama kuna tatizo lolote. Husimamia na kuwatunza wanawake wanaojifungua, huhakikisha wanajifungua salama na kuwatia moyo katika kila hatua. Mara baada ya mtoto kuzaliwa hukaushwa, husafishwa njia yake ya mfumo wa hewa, na mtoto kuwekwa kwenye tumbo la mama ili uwepo mgusano wa ngozi ya mama na mtoto. Ndani ya dakika moja, kitovu hukatwa na mama huchomwa sindano za kusaidia tumbo kusinyaa na maziwa kutoka kwa wingi ili kusaidia katika hatua ya tatu za kuzaa – kutoa kondo la nyuma la uzazi.

Hofne hushughulika na hatua hiyo ya tatu ya kuzaa ili kupunguza hatari ya kupoteza damu nyingi kwa sababu ya kuzaa. Kunapotokea matatizo,

yeye huzungumza na mgonjwa kuhusu kinachofuatia na kama kuna ulazima, haraka chumba cha upasuaji huandaliwa. Mifumo iliyowekwa ili kukabiliana na matatizo ya uzazi katika kambi hizi yanafanya kazi sawsawa na kuokoa maisha.

Abdul hutoa huduma za baada ya kuzaa, akisimamia uzito wa watoto wachanga na kukamilisha ukaguzi kamili wa mama na mtoto. Akina mama wanapaswa kwenda kliniki mara tatu baada ya kujifungua: siku ya 7, siku ya 28 na siku ya 42 ambapo watoto wachanga huanzishiwa ratiba ya chanjo ya kinga. Vipindi vya elimu ya afya pia hutolewa kwa akina mama katika kituo hicho. Mada kuu huwa ni uzazi wa mpango, lishe na matunzo ya mtoto.

Hofne na Abdul wanaokoa maisha na kuwawezesha wanawake na wasichana kupata afya ya ngono na uzazi na haki ya kuamua kama wanataka kupata watoto, wakati gani na kwa idadi ipi na kuhakikisha kwamba wale wanaozaa basi wanafanya hivyo kwa usalama. Mwaka 2018, asilimia 97 ya wanawake wajawazito katika kambi hizo tatu za wakimbizi walizaa katika kituo cha afya chini ya uangalizi wa wataalamu wenye mafunzo wa matunzo ya afya.

UNFPA itaendelea kutoa huduma zinazookoa maisha na afya ya uzazi wakati wote wa hatari kubwa na awamu ya uponyaji katika dharura za kiutu huko Kigoma, na kuhakikisha kwamba hakuna atakayeachwa nyuma.

RIPOTI MAALUMU I: UN, Serikali Zahusisha Vyama vya Kiraia kuhusu SDGs



Picha zote na *Lisa Brown/UN Tanzania*

Sekta binafsi, vyama vya kiraia, vijana, washirika wa maendeleo, na maafisa wa UN wakihamasisha Malengo ya Dunia wakati wa VNR huko Zanzibar

Mwezi Machi, serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Uchumi na Jamii (UN DESA), UN Tanzania na vyama vya kiraia iliandaa warsha ya mashauriano ya Mapitio ya Hiyari ya Kitaifa (Voluntary National Review (VNR)) kwa upande wa Bara na Visiwani na kupokea michango kutoka kwa wadau wasio wa kiserikali kuhusu hatua zilizopigwa katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) nchini Tanzania.

Warsha hizo ziliwaleta pamoja washiriki wa aina tofauti kuanzia maafis wa serikali na wadau wakiwemo vyama vya kiraia, mashirika yasiyo ya kiserikali,

sekta binafsi, wasomi, wanawake na vikundi vya vijana. Warsha hizi zilitoa fursa ya kujadili utendaji mzuri, changamoto, upungufu na fursa kuhusiana na utekelezaji wa SDGs nchini Tanzania.

Kwa upande wa Zanzibar, mashauriano yalihudhuriwa na taasisi mbalimbali zikiwemo Tume ya Mipango ya Zanzibar (ZPC) na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Zanzibar (ANGOZA) na wadau wengine.

Katibu Mtendaji kutoka ZPC, Bw. Juma Reli, alieleza kwamba lengo kuu la warsha hiyo lilikuwa kuhamasisha umiliki wa kitaifa na ushiriki kamlifu wa wadau muhimu huku kukiwa na

ongezeko la uwajibikaji katika utekelezaji na utoaji taarifa kuhusu SDGs. Pia alionyesha kwamba warsha hiyo ilikuwa ni fursa ya kubaini masuala yanayoibuka na vipaumbele ambavyo vingepaswa kuzingatiwa kwa ajili ya kutoa msaada zaidi katika kulenga MKUZA III na Ajenda 2030.

Jijini Dar es Salaam, warsha ulihudhuriwa na wadau wengi wakiwemo kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Idara ya Taifa ya Takwimu (NBS), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Ufilantropia ya Afrika (African Philanthropic Foundation), Taasisi ya Utafiti

Inaendelea ukurasa wa 9

Inatoka ukurasa wa 8

na Maendeleo (REPOA) na mashirika mengineyo.

Mratibu Mkazi wa UN Tanzania, Bw. Alvaro Rodriguez, alisisitiza kwamba VNR inapaswa kutumiwa kama njia ya kuongeza ufanisi katika uratibu wa SDGs. “Ni muhimu kukumbuka kwamba VNR siyo lengo lenyewe bali inatoa jukwaa la kuimarisha ushirika unaohitajika kufikia malengo makubwa yaliyoainishwa katika Ajenda ya 2030. VNR inapaswa kutumiwa ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa SDGs miongoni mwa wahusika wote,” alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Bw. Servus Sagday, alisema kwamba “manufaa itakayopata Tanzania kwa kuwasilisha VNR ni kwamba inaisaidia Tanzania kujifunza

kutoka katika nchi nyingine huku ikichangia kuwaleta watu pamoja katika mchakato wa pamoja na jumuishi tangu mwanzo hadi mwisho. Vyama vya kiraia na sekta binafsi ni muhimu na zinahitajika kushiriki katika mchakato.” Aliongeza kwamba rasimu ya ripoti ya VNR imeandaliwa kwa kushirikiana na wadau kutoka sekta binafsi na vyama vya kiraia na kwamba mchakato huo unahitaji ushiriki wa wadau wote wanaojihusisha na ajenda ya maendeleo, yaani, hakuna yeyote anayepaswa kubaki nyuma.

Michango ya warsha zote mbili utaonekana katika Mapitio ya Hiyari ya Taifa katika utekelezaji wa SDGs ambayo yatawasilishwa mwezi Julai wakati wa Jukwaa la Kisiasa la Ngazi ya Juu katika Makao Makuu ya UN jijini New York.

“manufaa itakayopata Tanzania kwa kuwasilisha VNR ni kwamba inaisaidia Tanzania kujifunza kutoka katika nchi nyingine huku ikichangia kuwaleta watu pamoja katika mchakato wa pamoja na jumuishi tangu mwanzo hadi mwisho. Vyama vya kiraia na sekta binafsi ni muhimu na zinahitajika kushiriki katika mchakato.”

**- Bw. Servus Sagday,
Mkurugenzi Msaidizi
Wizara ya Fedha na
Mipango**



Mkurugenzi Msaidizi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Bw. Servus Sagday, akitoa hotuba ya ufunguzi wakati wa mashauriano ya Mapitio ya Kitiifa ya Hiyari (VNR). Alisisitiza umuhimu wa vyama vya kiraia na sekta binafsi kushiriki katika mchakato wa VNR.

RIPOTI MAALUMU I: UN, Serikali Zahusisha Vyama vya Kiraia kuhusu SDGs



Sekta binafsi, vyama vya kiraia, vijana, washirika wa maendeleo, na maafisa wa UN wakihamasisha Malengo ya Dunia wakati wa VNR huko Zanzibar.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Ufilanthropia wa Afrika, Bw. Stephen Chacha (left); Mratibu wa Mtandao wa Dunia Moja wa UN (UNGC), Bw. Emmanuel Nnko; na mwezeshaji Bi. Maria Sarungi wakijadili umuhimu wa sekta binafsi na vyama vya kiraia kushirikiana. Hii ilikuwa wakati wa majadiliano kuhusu mashauriano ya Mapitio ya Kitaifa ya Hiayari (VNR) jijini Dar es Salaam.

RIPOTI MAALUMU I: UN, Serikali Zahusisha Vyama vya Kiraia kuhusu SDGs



Wajumbe kutoka sekta binafsi, vyama vya kiraia, taasisi za vijana, washirika wa maendeleo wakishiriki katika warsha ya VNR.



Maofisa wa Serikali na UN wakichukua picha ya pamoja na wadau kutoka vyama vya kiraia wakati wa mashauriano ya Mapitio ya Kitaifa ya Hiyari (VNR) yaliyofanyika huko Zanzibar mwezi Machi.

RIPOTI MAALUMU II:

Siku ya Kimataifa ya Wanawake: Serikali yatoa wito wa kupanua uwezeshaji wanawake kiuchumi



Picha zote na *Edgar Kiliba/UN Tanzania*

(Kutoka kulia kwenda kushoto) Mwakilishi wa UN Women, Bi. Hodan Addou; Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mh. Umyy Mwalimu; na Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Mh. Anders Sjöberg, wakikutana na mjasiriamali mwanamke kwakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake jijini Mwanza.

Kwa sherehe za mwaka huu za Siku ya Kimataifa ya Wanawake, Serikali ya Tanzania ilitenga siku nane za kuwapongeza wanawake kote nchini kupitia ujumbe wa taifa: 'Badili Mtazamo ili Kuleta Usawa katika Maendeleo Endelevu'. Katika mikoa kote nchini, ikiwemo Dodoma, Arusha na Kigoma na upande wa Zanzibar, wanawake na wasichana walizungumza na kushiriki katika maandamano ili kutambuliwa kama washirika wenye haki ya kuwa sawa katika maendeleo na kudai kuheshimiwa kwa haki yao ya kufurahia maisha yasiyo na unyanyasaji na ukatili wowote.

Kwa hakika ulikuwa na wasaa wa kufurahisha sana kwa

wanawake walio katika biashara ambao walitumia fursa hiyo kuonyesha biashara zao.

Moja ya taasisi zinazoendeshwa na wanawake ambayo iliibuka kinara ni ya kutoka Mwanza, Wanawake Wavuvi Maendeleo Nyamagana. Siyo tu kwamba kundi hili linauza samaki bora ndani na nje ya Mwanza, balil hivi karibuni walianza kutengeneza bidhaa kama vile vyakula vya kuku kutokana na mifupa na ngozi zilizokaushwa za samaki. Wanaunza bidhaa hizi kote nchini na hata katika baadhi ya nchi za jirani.

Mjasiriamali mwingine, Bi. Anchila Petro alivutia kundi kubwa kwa mvinyo wake

mwekundu wa kutengenezwa nyumbani kutumia Rosela. Bi. Petro, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kikundi Cha Upendo-Nyamatala Wineries aliamua mwaka 2014 kutengeneza mvinyo mwekundu kwa kutumia mmea wa Rosela ambao huuotesha shambani mwake. Baada ya kujifunza kuzalisha mvinyo, alianza kidogokidogo kujenga biashara yake kutokea nyumbani mwaka 2015, ambapo alizalisha tu lita 50 kwa mwezi.

Hivi sasa, Bi. Petro anazalisha hadi lita 200 za mvinyo bora mwekundu kwa mwezi. Bidhaa hii pia ilikuwepo na kuonyeshwa katika maadhimisho ya Siku

Inatoka ukurasa wa 12

ya Kimataifa ya Wanawake, ambayo ilifanyika mkoani Mwanza. Alifanikiwa kuuza chupa 60 katika maonyesho hayo. Bi. Petro ni miongoni mwa wanawake ambao mwaka jana walipata msaada wa kifedha kutoka serikalini ili kupanua biashara zao mkoani Mwanza.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mh. Ummy Mwalimu, alikuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo ya Bujora, mkoani Mwanza. Wengine walioshiriki ni wawakilishi wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania; Balozi wa Sweden, Mh. Anders Sjoberg; Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez; Mwakilishi wa UN Women, Bi. Hodan Addou; maafisa wa serikali; na, wawakilishi wa vyama vya kiraia. Wajumbe walibadilishana mawazo na wanawake wafanyabiashara, walitazama



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mh. Ummy Mwalimu akitoa hotuba wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake jijini Mwanza. Aliziagiza mamlaka zote za mikoa kuhakikisha wanayapa makundi ya wanawake mikopo ya kutosha ili kuhamasisha uwezeshaji wanawake kiuchumi.

“Wanawake na wasichana hawapaswi tu kuwa watumiaji wa kazi za ubunifu bali wao pia hawana budi kuwa wabunifu. Kupitia ushiriki wao, kwa usanifu na utekelezaji wa masuluhisho, wanaweza kushughulikia mahitaji muhimu. Haya ni kuanzia kuundwa kwa ajira hadi bidhaa, huduma na miundombinu kwa ajili ya wanawake wote,”

**- Bi. Hodan Addou,
Mwakilishi wa Nchi wa UN
Women**

bidhaa na kusikiliza kuhusu mafanikio na changamoto.

Katika hotuba yake, Waziri Mwalimu alisisitiza msaada zaidi kwawanawakewanaoshughulika na biashara ili kupanua biashara hizo, jambo ambalo litasaidia katika kutengeneza ajira. Wizara imekwishatangaza sera mpya, Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, ili kuhakikisha wanatekeleza njia mpya za ubunifu ili kusaidia wanawake walio katika biashara kukuza biashara zao.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa UN Women, Dkt. Phumzile Mlambo-Ngcuka, Mwakilishi wa Nchi wa UN Women, Bi. Hodan Addou,

aliwapongeza wanawake kwa ubunifu wao mkubwa katika biashara kote nchini. Alisema kwamba kuna haja ya kuchukua vitendo vya makusudi kuhusu matumizi ya ubunifu ili kuwezesha matokeo chanya katika maisha ya wanawake na wasichana.

“Wanawake na wasichana hawapaswi tu kuwa watumiaji wa kazi za ubunifu bali wao pia hawana budi kuwa wabunifu. Kupitia ushiriki wao, kwa usanifu na utekelezaji wa masuluhisho, wanaweza kushughulikia mahitaji muhimu. Haya ni kuanzia kuundwa kwa ajira hadi bidhaa, huduma na miundombinu kwa ajili ya wanawake wote,” alisema Bi. Addou.

RIPOTI MAALUMU II:

Siku ya Kimataifa ya Wanawake: Serikali yatoa wito wa kupanua uwezeshaji wanawake kiuchumi



Amani Girls Home, ambalo ni shirika lisilo la kiserikali la ndani linalowajengea wasichana uwezo ili kupata maendeleo endelevu, wakishiriki katika maandamano ya usawa wa jinsia wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake jijini Mwanza. Bango walilobeba lina ujumbe usemao: 'Usawa ni jambo ninalotaka, Ukatili dhidi ya wasichana na wanawake si ninachokitaka'.



Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake yaliyofanyika jijini Mwanza yaliwaleta watu mbalimbali kusherehekea wanawake na kutoa michango yao kwa maendeleo ya Tanzania. Ujumbe mkuu katika maadhimisho ya mwaka huu ni: *Badili Mtazamo ili Kuleta Usawa wa Jinsia kwa ajili ya Maendeleo Endelevu.*

Rais Shein atoa tuzo kwa Wahitimu wa Programu ya Uanagenzi ya ILO



Wahitimu wa Uanagenzi kutoka Chuo Kikuu cha Serikali cha Zanzibar (SUZA) wakiwa katika siku yao ya mahafari. **Picha | ILO**

Mwishoni mwa Aprili, wanagenzi 52 walijiandikisha kwa ajili ya programu ya Uanagenzi wenye Ubora Zanzibar mwaka 2017 katika Chuo Kikuu cha Serikali cha Zanzibar (State University of Zanzibar (SUZA)). Kati ya wahitimu 52, wahitimu 24 walipata vyeti vya Kuhudumia Dawati la Mapokezi, 16 katika Uzalishaji wa Chakula na Uoakaji na 12 katika Huduma za Vyumbani. Wahitimu wameiva kwa ajira zenye tija zaidi ambapo 33 kati yao tayari walipata kazi katika hoteli mbalimbali hata kabla ya kumaliza mafunzo yao ya uanagenzi.

Makamu Mkuu wa SUZA, Prof. Idris Rai alilipongeza Shirika la Kazi Duniani (ILO), serikali na washirika katika uendeshaji wa programu hiyo na kwa kutekeleza programu ya kwanza iliyotoa veyti kwa wanagenzi huko Zanzibar. “Programu hii ya Uanagenzi ya ILO inasaidia

kutoa mafunzo kwa vijana wa kiume na kike wanaotaka kujiunga katika sekta ya utalii. Kama tunavyojua, utalii ni muhimu sana kwa maendeleo yetu ya kiuchumi na ni muhimu kwa vijana kupata ujuzi stahiki kadiri ya mahitaji ya sekta hii,” Prof. Rai alisema.

Rais wa Zanzibar, Mh. Dkt. Ali Mohamed Shein—ambaye pia ndiye Mkuu wa Chuo cha SUZA—aliimwagwa sifa programu hiyo na kumtunuku Mwanagenzi Saada Mzee kwa Tuzo ya Makamu Mkuu wa Pili wa Chuo ya mwanafunzi bora katika programu zote za cheti kwa mwaka 2017/2018.

Bw. Jealous Chirove, Mtaalamu wa Ajira wa ILO, akiongea katika tukio hilo kwa niaba ya Mkurugenzi wa ILO, Ofisi ya Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi, Bw. Wellington Chibebe, aliwaasa wahitimu wapya kufikiri kuhusu maisha ya kazi na kuendelea

kuongeza ujuzi wao ili kuwa na nafasi kubwa zaidi kwa kila fursa. “Msisitizo ni kuwa kujifunza liwe ni jambo la maisha yote. Tunatafuta njia za kuwasaidia na kuwapa mafunzo, lakini ni wajibu wenu kutumia vyanzo mbalimbali hasa vya mtandaoni ili mwendelee kujifunza,” alisema.

Kwa ufadhili wa kutoka Serikali ya Norway, Programu ya Uanagenzi Bora katika Uendeshaji wa Hoteli ulizinduliwa rasmi mwezi Agosti 2017 na ndiyo programu ya kwanza ya uanagenzi kuthibitishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi la Tanzania (NACTE). Hii pia ni mara ya kwanza kwa SUZA kutambua na kutoa vyeti vya uanagenzi kamam moduli yenye ithubati ya kujifunza. Nafasi za wanagenzi waliohitimu zinajazwa na wanagenzi wapya 150 wanaotarajiwa kuanza masomo yao mwezi Mei, 2019.

WFP yakabidhi mashine ya nafaka yenye thamani ya \$170,000 kwa Serikali



Mwakilishi wa Nchi wa WFP, Bw. Michael Dunford (kushoto), na Waziri wa Kilimo, Mh. Japheth Hasunga (kulia) wakishiriki katika sherehe za kukabidhi mashine za kusafisha mahindi zilizotolewa na WFP kwa Wizara. *Picha | Alice Maro WFP*

Katikati ya mwezi Machi, Mpango wa Chakula Duniani (WFP) lilikabidhi mashine ya kusafisha nafaka kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). Hafla

hiyo ilihudhuriwa na Waziri wa Kilimo, Mh. Japheth Hasunga; Kaimu Mtendaji Mkjuu wa NFRA, Bi. Vumilia Zikankuba; na Mwakilishi wa Nchi wa WFP, Bw. Michael Dunford.

Mashine hiyo ya kusafisha nafaka, yenye thamani ya Dola za Marekani 170,000, ina uwezo wa kuchakata tani za metriki 12-18 kwa saa na kuiwezesha NFRA kusafisha mahindi kwa haraka zaidi kuliko njia za hapo zamani. Mashine hiyo pia inahakikisha kwamba takataka na vyote visivyohitajika vinaondolewa kwa kiasi kikubwa na hivyo kupunguza hatari ya maambukizi na hasara.

Mahitaji ya WFP kwa ajili ya operesheni za kiutu na maendeleo Mashariki na Kusini mwa Afrika zinatoa fursa ya kununua mahindi kutoka Tanzania. Jambo hili lina manufaa kwa wakulima wadogowadogo kwa kuwapa masoko kwa bidhaa zao (kupitia NFRA).

Kutomwacha kijana yeyote nyuma nchini Tanzania

Mashauriano ya Vijana ya Mapitio ya Taifa ya Hiyari kwa Tanzania kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) yalifanyika jijini Dar es Salaam mnamo tarehe 28 Machi, 2019, chini ya ujumbe: 'Kutomwacha Kijana Yeyote Nyuma'. Tanzania imejitolea kuwasilisha VNR yake mbele ya Jukwaa la Ngazi ya Juu la Kisiwa mwezi Julai, 2019—hatua ambayo ni nzuri kueleka katika utekelezaji SDGs ulio jumuishi. Jukwaa hilo ndiyo daraja kuu la Umoja wa Mataifa kuhusu maendeleo endelevu na lina jukumu kuu la kufuatilia na kufanya mapitio ya SDGs katika ngazi ya dunia.

Mashauriano hayo yaliandaliwa na Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Idadi ya Watu (UNFPA) kwa



Mashauriano ya Vijana kuhusu Mapitio ya Kitaifa ya Hiyari (VNR) juu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu yaliwaleta pamoja vijana kutoka michango yao kuhusu utekelezaji wa SDGs. *Picha | UNFPA*

kushirikiana na Chama cha Umoja wa Mataifa (UNA), kwa kushirikiananataasisiza Restless Development, Mulika Tanzania na AfriYAN, na kuwakaribisha

wawakilishi 50 kutoka katika vikundi vinavyoongozwa na kuwahudumia vijana katika maeneo mbalimbali Tanzania

Inatoka ukurasa wa 15

Bara na Zanzibar. Uwakilishi wa ngazi ya kanda/mikoa ulihakikisha kwamba sauti za vijana wengi zaidi zinasikika.

Mashauriano ya vijana, yaliandaliwa ili kuhimiza ujumbe wa 'Kutomwacha Yeyote Nyuma' wa SDGs, kwa kulenga ushiriki unaofaa wa vijana katika utekelezaji wa SDGs kwa kuweka mkazo katika Malengo ya 3, 4, 5, 8, 10 na 16. Mashirika yanayoongozwa na kuhudumia vijana yalishirikisha uzoefu wao, mafanikio na pia yale wanayoona

kuwa ni changamoto katika utekelezaji wa SDGs.

Ajenda ya 2030 na SDGs haziwezi kufikiwa pasipo ushiriki kamilifu na ushirikishwaji wa vijana wa Tanzania. Wakati ambapo mara nyingi vijana wanaathiriwa kwa namna isiyo sawa na masuala yaliyoainishwa katika SDGs, wote wana nafasi nzuri ya kutafuta ufumbuzi wake. Akizungumza na washiriki katika warsha, Kaimu Mwakilishi wa Nchi wa UNFPA, Dkt. Hashina Begum, alitoa wito kwa vijana kuitafsiri dunia ambamo kwamo

wanaishi na kuleta mabadiliko kwenye dunia watakayoirithi ifikapo mwaka 2030, akiongeza: "Hatuwezi daima kujenga hatima ya vijana wetu, lakini tunaweza kuwaandaa vijana wetu hatima hiyo ijayo. Vijana wanapaswa kuwa kiini cha Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu na kuleta mabadiliko chanya duniani."

Msaada wa UNFPA kwa mchakato wa VNR ni mwendelezo wa juhudi za tangu siku za nyuma wa kuendeleza nafasi na wajibu wa vijana katika utekelezaji wa SDGs.

Mkutano wa Ushirika wa UN, Serikali kuhusu msaada wa ukuaji wa kiuchumi na ajira Tanzania



(kutoka kushoto kwenda kulia) Mwakilishi wa Nchi wa UNIDO, Mh. Steven Kargbo; Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez; na Mwakilishi Mkazi wa UNDP, Bi. Natalie Boucly, wakiwa katika mkutano wa kujadili Ukuaji wa Kiuchumi na Matokeo ya Ajira. **Picha | ILO**

Matokeo ya Kimaudhui la Ukuaji Jumuishi, Mwakilishi Mkazi wa UNDP, Bi. Natalie Boucly, alisisitiza umuhimu wa UN kuisaidia Tanzania kufikia ukuaji jumuishi kupitia kuongezwa kwa ajira zenye hadhi, kupanua kinga ya jamii na kuimarisha ubora wa elimu. Aliendelea kwa kuipongeza Serikali kwa ushirika wake na utayari wake wa kufikia ukuaji jumuishi. Hili lilirudiwa na Mratibu Mkazi wa UN Tanzania, Bw. Alvaro Rodriguez, ambaye alisisitiza zaidi nafasi ya Lengo la 8 katika SDGs kuhusu Kazi zenye Hadhi na Ukuaji wa Kiuchumi ili kumaliza umaskini mkali, kwa kuweka mkazo katika kuhamasisha ukuaji wa kiuchumi unaoendana na upatikanaji wa nafasi nyingi za kazi.

Katikati mwa mwezi Machi, Kundi la Ukuaji wa Uchumi na Matokeo ya Ajira katika eneo la kimaudhui la Ukuaji Jumuishi katika Mpango wa Pili wa Msaada wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDAP II) liliandaa mkutano wa ushirika uliopata ushiriki mkubwa wenye

lengola kuhakikisha mwendelezo wa umiliki wa utekelezaji wa UNDAP II na uratibu bora wa hatua zinazochukuliwa na UN/Serikali katika kuhimiza ukuaji wa kiuchumi na ajira.

Katika hotuba yake ya ufunguzi, Mwenyekiti wa Kundi la

Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango ya Zanzibar, Bw. Juma Reli, aliipongeza UN kwa kuwa mshirika mwaminifu na wa kutegemewa katika kuhamasisha ajenda ya taifa ya maendeleo, na aliangazia mafanikio muhimu katika

Inaendelea ukurasa wa 18

Inatoka ukurasa wa 17

kuhamasiha ukuaji jumuishi.

Katika uwasilishaji kuhusu mafanikio muhimu, Mratibu wa Ukuaji wa Uchumi na Matokeo ya Ajira, Bi. Kristina Weibel, alisisitiza msaada katika sera za maendeleo zinazotokana na utafiti na mipango ya utendaji na pia kujenga uwezo, ambayo yote yanasababisha utendaji bora wa taasisi za serikali na sekta binafsi. Vilevile, alianganzia msaada katika uendelezaji wa mnyororo wa thamani ambao ulisababisha zaidi ya biashara 51,000 (asilimia 44, wanawake) baada ya kukuza uwezo wao wa kuzalisha na vipato vyao.

Walau washiriki 40 walihudhuria mkutano huo, wakiwemo Ubalozi wa Sweden ambao unasaidia Kundi la Matokeo kupitia Mfuko wa Pamoja.



Maofisa wa UN wakishiriki katika mkutano wa washirika wa Ukuaji wa Uchumi na Matokeo ya Ajira. *Picha | ILO*

Washiriki walikubaliana kuhusu vipaumbele vya kimkakati vifuatavyo: kuendeleza ujuzi maalumu; kuhamasisha ujenzi wa uchumi wa viwanda na uwekezaji; mshikamano wa sera; ubunifu; na uendelezaji wa mnyororo wa thamani. Wito

ulitolewa kwamba mkutano kama hiyo iandaliwe kwa ajili ya Makundi ya Kinga ya Jamii na Matokeo ya Elimu, ambayo yanaunda shemu ya eneo la kimaudhui la Ukuaji Jumuishi la UNDAP II.

WFP yatiliana saina makubaliano yenye thamani ya \$600,000 na Shirika la Reli la Tanzania



Mkurugenzi Mtendaji wa TRC, Bw. Masanja Kadogosa (kulia); Waziri wa Kazi, Usafirishaji na Mawasiliano, Mh. Inj. Isaac Kamwelwe (katikati); na Mwakilishi wa Nchi wa WFP, Bw. Michael Dunford (kushoto) wakionyesha Makubaliano ya Mkatoba kwa ajili ya kukarabati mabehewa 40 ya treni. *Picha | Alice Maro/WFP*

Katikati ya mwezi Machi, Mpango wa Chakula Duniani (WFP) lilitiliana saina makubaliano (MoU) na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa ajili ya ukarabati wa

mabehewa 40 kwa thamani ya Dola za Marekani 600,000. Makubaliano hayo yalitwa saina na Mkurugenzi Mtendani wa TRC, Bw. Masanja Kadogosa, na Mwakilishi wa Nchi wa WFP,

Bw. Michael Dunford.

Wakati wa hafla hiyo, Bw. Dunford alisisitiza kwamba WFP itaendelea kuunga mkono Serikali katika juhudi zake za kujenga uchumi wa viwanda na kuwasaidia watu wa Tanzania. Kauli hii ilipokewa vema na Waziri wa Kazi, Usafirishaji na Mawasiliano, Mh. Inj. Isaac Kamwelwe, ambaye aliipongeza WFP kwa msaada inaoendelea kuutoa kwa Tanzania.

Utaratibu huo unawakilisha ushindi kwa kila upande, ambapo TRC itapata mabehewa yaliyokarabatiwa, kuimarisha mahitaji ya uendeshaji operesheni za kiutu katika ukanda na kuongeza uwezo wakati ambapo WFP itaokoa fedha kwa matumizi ya mara kwa mara ya usafirishaji kwa njia ya reli.

UNDP yajenga suhula za maji na usafi wa mazingira zenye thamani ya \$100,000 kwa shule 4 za msingi mkoani Iringa



Vyoo vya kisasa ambavyo vilijengwa na menejimenti na mamlaka za serikali za mitaa kupitia msaada kutoka UNDP vitachangia katika kuimarisha mazingira bora na safi zaidi ya shule, jambo litakalosaidia kupatikana kwa usawa na utoaji wa elimu bora kwa wanafunzi—hasa wasichana. **Picha | Edgar Kiliba/UN Tanzania**

Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) limetumia Dola za Marekani 100,000 kwa ajili ya suhula za maji na usafi wa mazingira (WASH) katika shule nne za mkoani Iringa. Suhula hizo zilizinduliwa mwezi Machi na Waziri wa Katiba na Mambo ya Sheria, Mh. Dkt. Augustine Mahiga; Mratibu Mkazi wa UN., Bw. Alvaro Rodriguez; Mwakilishi Mkazi wa UNDP, Bi. Natalie Boucly na pia viongozi mbalimbali wa serikali katika ngazi ya mkoa. Vyoo hivyo vilijengwa na mamlaka za mkoa na menejimenti za shule na vinatarajiwa kuchangia mazingira bora na safi zaidi ambayo yatasaidia kutoa elimu jumuishi na yenye kutoa haki zaidi kwa wanafunzi.

UNDP Tanzania iliisaidia Sekretariati ya Uongozi wa Mkoa wa Iringa kwa Dola za Marekani 100,000 ili kujenga suhula za

maji na usafi wa mazingira katika shule nne ili kuhakikisha kwamba kuna miundo mbinu ya kutosha ya usafi wa mazingira kwa wavulana na wasichana na pia kwa ajili ya walimu. Baada ya kukamilika, suhula hizo zitahudumia wanafunzi 1,900—miongoni mwao 842 wakiwa wasichana na wavulana 1,085. Zaidi ya hayo, suhula hizo za wavulana na wasichana zina vyumba maalumu kwa ajili ya watoto wenye ulemavu. Kwa kuongezea, kila suhula ya wasichana ina chumba maalumu kwa ajili ya matumizi yao wanapokuwa kwenye hedhi.

Waziri Mahiga alisisitiza umuhimu wa maji safi na salama na mazingira safi na kuwaambia wanafunzi kwamba licha ya yale wanayojifunza darasani, ni muhimu pia kujifunza masuala yanayohusiana na afya njema

na hali njema ya afya, ikiwemo matumizi sahihi ya vyoo.

Kwa upande wake, Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez,

“Kukosekana kwa suhula sahihi ni moja ya changamoto kubwa zinazozikabili shule na hasa kuwaumiza wasichana zaidi. Kwa namna ya pekee, wasichana, watakuwa na changamoto kidogo wanapohudhuria shule. Wakati huohuo, usafi utaimarika, na hii maana yake ni kuwa na wanafunzi na familia zenye afya bora zaidi.”

**- Bw. Alvaro Rodriguez
Mratibu Mkazi wa UN**

Inaendelea ukurasa wa 20



Waziri wa Katiba na Mambo ya Sheria, Mh. Dkt. Augustine Mahiga (kulia) akitembezwa katika moja ya vyoo vilivyojengwa hivi karibuni. Nyuma yake (kutoka kulia kwenda kushoto) ni Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez, na Mwakilish Mkaziwa UNDP, Bi. Natalie Boucly.

Picha | Edgar Kiliba/UN Tanzania

Siku za Umoja wa Mataifa

Mei 22 - Siku ya Kimataifa ya Uanuwai wa Kibaiolojia

Mei 23 - Siku ya Kimataifa ya Kusaliza Tatizo la Fistula

Mei 29 - Siku ya Kimataifa ya Walinda Amani wa UN

Juni 5 - Siku ya Mazingira Duniani

Juni 8 - Siku ya Bahari Duniani

Juni 13 - Siku ya Kujenga Uelewa wa Watu wenye Ualbino

Juni 14 - Siku ya Dunia ya Wanaojitolea Damu

Inatoka ukurasa wa 19

alipongeza mradi wa UNDP na ushirika uliokuwapo na serikali na shule za mahalia na kwamba jambo hili lote linamaanisha hatua moja zaidi katika kuhamasisha maendeleo endelevu, kuimarishwa kwa suhula za wavulana na wasichana, na kuimareisha uwezekano wa kufikiwa kwa Malengo ya Dunia ifikapo mwaka 2030. “Kukosekana kwa suhula sahihi ni moja ya changamoto kubwa zinazozikabili shule na hasa kuwaumiza wasichana zaidi. Kwa

namna ya pekee, wasichana, watakuwa na changamoto kidogo wanapohudhuria shule. Wakati huohuo, usafi utaimarika, na hii maana yake ni kuwa na wanafunzi na familia zenye afya bora zaidi.”

Kwa upande wake, Mwakilishi Mkaziwa UNDP, Bi. Natalie Boucly, alisema kwamba: “Ninaamini mradi huu wa UNDP utaimarisha usafi wa maji na mazingira katika shule zilizolengwa na kuwapatia wanafunzi mazingira bora ya kujifunza—hasa wasichana na watu wanaoishi na ulemavu.”

Umoja wa Mataifa Madhubuti kwa Dunia Bora Zaidi !



**UNITED NATIONS
TANZANIA**



**United Nations
Resident Coordinator's Office**

Phone: (+255) 22-219-5021

Website: www.tz.one.un.org



Kwa taarifa zaidi tembelea: tz.one.un.org